

MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA APRILI, 2018 NA MWELEKEO WA MEI, 2018

Dondoo za Mei, 2018

Taarifa hii inatoa muhtasari wa hali ya viashiria vya hali ya hewa na mwenendo wa mvua katika mwezi wa Aprili, 2018 na mwelekeo wa viashiria na hali ya mvua kwa mwezi Mei, 2018 nchini.

- a) Mvua za '*Masika*' katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka zinatarajiwa kupungua kuelekea wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Mei, 2018.
- b) Mvua za '*Msimu*' katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka zinaelekea kuisha katika maeneo mengi, hata hivyo kuna uwezekano wa mvua nyepesi hususan katika maeneo yenye miinuko pamoja na maeneo ya kati mwa nchi.

1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI APRILI, 2018 NA MATAZAMIO KWA MWEZI MEI, 2018.

1.1 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI APRILI, 2018

Katika kipindi cha wiki tatu za mwanzo za mwezi Aprili, kulikuwa na mtawanyiko wa kuridhisha wa mvua kubwa katika maeneo mengi hapa nchini, hata hivyo viwango vikubwa kwa siku vya mvua vilipimwa katika vituo vilivyopo pwani ya kaskazini (bandari ya Dar es salaam milimita 164.5 na milimita 115.3 katika kituo cha Zanzibar). Mfululizo wa mvua hizo katika maeneo ya pwani ya kaskazini ulisababisha uharibifu wa miundo mbinu ya barabara, majeruhi pamoja na vifo kadhaa.

2.0 MATAZAMIO MEI, 2018

2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Hali ya joto la chini ya wastani inatarajiwa katika eneo la kati la Kitropikali la bahari ya Pasifiki, na hali ya joto la juu ya wastani inatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi, Pwani ya Angola, pamoja na pwani ya Somalia. Hali hii ya joto la juu ya wastani linatarajiwa kuendelea kuushikilia ukanda wa mvua katika eneo la nchi yetu hivyo kusababisha mvua katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka katika kipindi cha mwezi Mei, 2018.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA MWEZI MEI, 2018

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Vipindi vingi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo hususan katika wiki ya kwanza na ya pili, ikifuatiwa na mvua za wastani katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): Upungufu wa mvua unatarajiwa katika maeneo mengi katika wiki ya kwanza ya mwezi, ikifuatiwa na ongezeko la mvua katika wiki ya pili ya mwezi Mei, 2018.

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): Vipindi vingi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo hususan katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Mei, ikifuatiwa na mvua za wastani katika wiki mbili za mwisho zilizosalia.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Vipindi kadhaa vya mvua vinatarajiwa katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Mei hususan katika mkoa wa Kigoma, mikoa mingine iliyobakia inatarajiwa kuwa na upungufu wa mvua kuelekea mwishoni mwa msimu.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Mvua za msimu zinapungua kuelekea mwishoni mwa msimu. Hata hivyo vipindi kadhaa vya mvua vinatarajiwa katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Mei, 2018.

Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Njombe, Iringa, Mbeya pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro): Mvua za msimu katika maeneo mengi zinaelekea kupungua. Hata hivyo vipindi kadhaa vya mvua vinatarajiwa katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Mei, 2018 kwenye maeneo ya miinuko.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Uwezekano wa mvua katika maeneo machache hususan katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi, ikifuatiwa na hali ya ukavu kuelekea mwishoni mwa msimu.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma): Uwezekano wa mvua katika maeneo machache hususan katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi, ikifuatiwa na hali ya ukavu kuelekea mwishoni mwa msimu.

Imetolewa na;

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA